Milenia Na Mwisho Wa Dhambi

“Milenia ni miaka elfu moja ya utawala wa kristo pamoja na watakatifu wake mbinguni kati ya ufufuo wa kwanza na pili. Wakati huo waovu waliokufa watahukumiwa, dunia itakuwa ukiwa na utupu, bila wanadamu wakazi walio hai, lakini ikikaliwa na shetani na malaika zake. Mwishowe kristo na watakatifu wake na Mji Mtakatifu watashuka kutoka Mbinguni. Ndipo waovu waliokufa watafufuliwa, nao pamoja na shetani na malika zake watauzingira mji, Lakini moto kutoka mbinguni utawateketeza ili kuitakasa dunia. Na hivyo ulimwengu utakuwa huru bila dhambi na wenye dhambi milele.” (Ufu. 20; 1Kor. 6:2-3, Yer. 4:23-26, Ufu 21:1-5; Mal 4:1; Eze 28:18-19)

Katika historia yote, wamekuwako watu wanaodai kwamba kuzimu kunatisha, wakiwajengea watu hofu ili kwa hofu hiyo watu wamwabudu Mungu. Je, ni Mungu wa namna gani wanayemtangaza? Hivi, hatimaye Mungu ataikomeshaje dhambi. Nini kitamtokea Shetani. Nini kitaifanya dhambi isijiinue tena? Hivi, inakuwaje Mungu mwenye haki awe pia Mungu mwenye upendo?

Matukio Kabla ya Miaka 1,000

Kipindi cha miaka 1,000 ambacho Ufunuo sura ya 20 huzungumzia, ushawishi wa Shetani katika dunia utazuiliwa na Kristo atatawala na watakatifu wake. (Uf. 20:1-4)

Kuja kwa Yesu Mara ya Pili

Ufunuo 19 na 20 hufuatana, hakuna palipoachana. Huelezea kuja kwa Yesu mara ya pili (Uf. 19:11 – 21) na papo kwa hapo huingiza miaka 1,000, ikimaanisha miaka 1,000 huanza Yesu akirudi mara ya pili. Kabla Yesu hajarudi, mamlaka tatu zitapinga kazi ya Kristo ambazo ni joka, mnyama na nabii wa uwongo (Uf. 16:13). Kuja kwa Yesu kutaangamiza washirika wawili (Uf. 19: 19, 20). Mshirika mwingine atashughulikiwa kwenye miaka 1,000. Ufalme wa Yesu hautakuwa wa ubia (Dan. 2:44).

Ufufuo wa Kwanza Ufu. 20:6 “Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri aliye na sehemu katika ufufuo huu.

Watakatifu watanyakuliwa kwenda mbinguni

Baada ya ufufuo wa wenye haki: watakatifu waliofufuliwa na watakaokutwa hai watanyakuliwa kumlaki BWANA hewani (1 Thes. 4:17) Pia, watakaribishwa mbinguni (Yoh. 14: 2, 3)

Maadui wa Kristo watakufa

Uf. 19: 21 Watauawa kwa upanga utokao kwa yule aketiye juu ya kiti kile cha enzi. Litakuwa ni jambo la ghafla kwao - kama ilivyokuwa siku za Nuhu, na siku za Sodoma (Mt. 24: 37-39 Luk. 17:29). BWANA anakuja kutoka mahali pake.. ili kuwaadhibu wakaao duniani… (Isa. 26:21).

Nchi itakuwa ukiwa

Kwa kuwa watakatifu watakuwa wamenyakuliwa na waovu kuangamizwa, dunia itabaki kwa kipindi haina wanadamu walio wakazi ndani yake. Yer. 4: 23- 25. Yeremia anatumia neno linalopatikana kwenye Mwa. 1:2 dunia ilikuwa utupu.

Shetani atafungwa

Kama mbuzi wa Azazeli alivyowekewa dhambi za Waisraeli, (Law. 16:21), alipelekwa porini (Law. 16:22). Shetani atafungwa kuzimu (Uf. 20:2, 3) yaani kwenye dunia iliyoharibiwa kwa kupondwa kwa mapigo saba (Uf. 16: 18 – 21).

Matukio Katika Miaka 1,000

Kristo mbinguni pamoja na Watakatifu

Watakatifu watakuwa na Kristo mbinguni. Kama Musa na Waisraeli wa zamani, watamshukuru Mungu kwa ukombozi nao wataimba wimbo wa Musa na Mwanakondoo Uf. 15:2, 3.

Watakatifu watatawala pamoja na Kristo

Watakatifu watakuwa mbinguni wakitawala na kupewa hukumu (Uf. 20: 4). Ashindaye… atapewa mamlaka juu ya mataifa. (Uf.2:26). Watakatifu watakuwa na ufalme, ukuu, mamlaka chini ya mbingu zote (Dan. 7:27).

Hukumu ya Waovu

Ufu. 20: 4 Watakatifu juu ya viti vya enzi wakihukumu. Shetani na malaika zake watahukumiwa (2 Pet. 2:4, Yuda 6,). Watakatifu watahukumu malaika kitatimia (1 Kor. 6: 1 – 3). Hukumu wanayofanya watakatifu siyo kuamua nani ataokolewa au kupotea. Hiyo itakuwa imefanywa na Mungu. Wao wataangalia kwa nini wanadamu wengine walinyimwa uzima na hilo litajenga imani kwa mamlaka ya Mungu katika mioyo yao.

Shetani atapata fursa kutafakari

Akiwa hana wa kudanganya, Shetani atanyong'onyea. Atatafakari chanzo cha dhambi na matokeo yake na sehemu aliyofanya kwenye shindano la wema na uovu. Atatafakari kwa hofu adhabu inayomstahili.

Siku za mwisho	**Miaka 1, 000**	**Umilele**
Kristo anarejea	***Ufufuo wa Kwanza***	***Ufufuo wa Pili***
Watakatifu wanyakuliwa		Yesu , watakatifu pamoja na mji washuka
Waovu waangamizwa (wabaki makaburini)	Watakatifu watawala na Kristo miaka elfu	Waovu waliokufa wanafufuliwa
Shetani afungwa	Wanachofanya ni kupitia hukumu	Shetani anafunguliwa apanga kushambulia mji mtakatifu
Dunia inabaki ukiwa (mapigo saba, tetemeko la Yesu kurudi mara ya pili)	Dunia inabaki ukiwa miaka elfu	Hukumu ya waovu yatekelezwa (Shetani, waovu, matokeo ya dhambi vyaangamizwa
		Dunia yafanywa upya kama maskani ya milele ya Watakatifu

Matukio Baada ya Miaka 1,000

Baada ya miaka 1,000, waovu watafufuliwa na Shetani atafunguliwa kutoka kwenye kifungo chake (Uf. 20: 5, 7). Atawadanganya kwamba waweza kuiteka kambi ya watakatifu ambayo itakuwa imeshuka pamoja na Yesu wakati huu (Uf. 20:9).

Kristo, watakatifu pamoja na mji mtakatifu washuka

Mji wa Yerusalemu mpya utashuka (Uf. 21:2). Yesu atatengeneza bonde, ambako mji huo utashukia (Zek. 14:4). Atakuwa mfalme wa dunia yote (Zek. 14:9)

Ufufuo wa waovu

Walioko makaburini wataisikia sauti (Yoh. 5:28) na kwa kuwa watakatifu walikwisha fufuliwa ufufuo wa kwanza wa uzima, safari hii ni ufufuo wa hukumu (Yoh. 5:29). Ufufuo wa wafu waliosalia (Uf. 20:5).

Kifungo cha Shetani kinakoma

Ufufuo wa waovu mwisho wa miaka 1,000 utamfungulia Shetani. (Uf. 20:3). Atathubutu kudanganya mataifa kwenye pembe nne za nchi (Uf. 20:8).

Jiji litazingirwa

Katika uwongo wake wa mwisho, Shetani atawatia moyo waovu kwamba wanaweza kuuteka ufalme wa Mungu kwa nguvu. (Uf. 20: 8, 9). Kutaka kumpindua Mungu, kutafanya tabia ya Shetani kudhihirika kwa wote.

Kiti kikubwa cheupe cha enzi

Yohana anasema aliona kiti kikubwa cheupe cha enzi ambako Mungu atahukumu (Uf. 20:11-15). Hapa ndipo Yesu aliposema watashangaa kumwona Ibrahimu, Isaka, Yakobo na manabii katika ufalme lakini wenyewe wametupwa nje (Luk. 13:28). Tutasimama wote mbele ya kiti cha hukumu (Rum. 14;10). Wema kwa waovu tutamsujudia Mungu (Wafil. 2:10, 11, Isa. 45:22, 23)

Shetani na waovu wataangamizwa

Baada ya kusomewa hukumu, Shetani, malaika zake na waovu watapata ijara yao. (Uf. 20:9, 12-15). Nje ya mji kunayeyuka na kuonekana ziwa la moto (2 Pet. 3:7), siku ya kisasi cha Mungu (Isa. 34:8) atakayofanya kitendo cha ajabu (Isa. 28:21). Kila asiyeonekana katika kitabu cha uzima alitupwa kwenye ziwa la moto (Uf. 20:15). Shetani naye atatupwa kwenye ziwa la moto (Uf. 20:10).

=====Mwisho wa Somo====

Adhabu Ya Waovu

Mafungu kadha wa kadha ya Biblia yanaweza kumsumbua msomaji wa kawaida akadhani kwamba adhabu ya waovu yawezekana kuungua moto milele pasipo kufa. Mafungu machache ni kama yafuatayo: -

Ondokeni kwangu mliolaaniwa mwende kwenye moto wa milele.... (Mt. 25: 41). Na hao watakwenda zao kuingia kwenye adhabu ya milele... (Mt. 25: 46). Watakapoangamizwa kwa maangamizi ya milele (2 Thes. 1: 9). Ziwa liwakalo moto na kiberiti (Uf. 21: 8). ...yeye naye atateswa kwa moto na kiberiti...na moshi wa maumivu yao hupanda juu milele hata milele. (Uf. 14: 9 – 11).

Hivyo yafaa kusoma somo hili, la hukumu ya waovu ili kuondoa dhana potofu inayoweza kutokeza

Hukumu / Adhabu ya waovu inasemwaje na Biblia?

Chanzo chema kwa ajili ya kuondoa shaka juu ya wazo linaloweza kuzuka, ni Maandiko matakatifu.

Hukumu ya waovu itatekelezwa wakati ujao, siyo sasa

Wako wanaoamini kwamba mtu akifa akiwa mwovu, hutupwa jehanamu. Wengine husema kwamba waovu hupata ijara yao hapahapa wakiwa hai. Inawezekana waovu wakaadhibiwa kwa kusutwa na jamii au hata kufungwa na Serikali au mamlaka. Lakini huo siyo adhabu kwa ajili ya dhambi. Ni adhabu kwa makosa yao ya jinai tu. Dhambi ni uhalifu dhidi ya sheria ya Mungu, hivyo itapatilizwa na Mungu mwenyewe, siyo mamlaka ya kidunia.

Hata malaika waliokosea hawajapata ijara yao. Yesu alipokuwapo duniani, mapepo yalipata kuuliza, je umekuja kutuhukumu kabla ya muhula wetu? (Mt. 8: 29). Malaika waovu wanalindwa hata ije hukumu (2Pet. 2: 4) au siku ya hukumu kuu (Yuda 9). Waovu watahukumiwa katika siku ya hukumu (2Pet. 2: 9).

Kinachofanya hukumu / adhabu ya waovu

1. *Waovu watakufa.* Roho itendayo dhambi itakufa (Ez. 18: 4). Mshahara wa dhambi ni mauti (Rum. 6: 23). Inasisitizwa kwamba adhabu wa waovu ni mauti. Waovu wanatajwa kuwa wanastahili mauti (Rum. 2: 31). Mwisho wa dhambi unatajwa ni mauti (Rum. 6: 21) na dhambi ikishakukomaa huzaa mauti (Yak. 1: 15).
2. *Waovu wataharibiwa.* Zab: 37: 9, 34. Katika Ezekieli 28: 16, neno kali zaidi limetumiwa, ‘kerubi ameangamizwa’.
3. *Waovu watapotea.* Watapotea (Zab. 37:20), watatoweka. Hawatakuwapo. (Zab. 37: 10) Watapotea usoni pa Mungu (Zab. 68: 2). Katika agano jipya, Yoh. 3: 16, inaunga mkono kuwa wasio mwamini Yesu watapotea.
4. *Waovu watachomwa moto.* Msemo mkali wa kuchoma moto umejirudia rudia pia.

   Angalia siku inawaka kama tanuru, haitaacha shina wala tawi (Mal. 4:1). Watafungwa matita matita na kuchomwa (Mt. 13:30), magugu yatachomwa (Mt. 13: 40). Petro naye anasema dunia na kazi zake zitachomwa (2 Pet. 3: 10). Kikomo cha mwisho cha waovu ni ziwa la moto (Uf. 20: 15). Hiyo ndiyo mauti ya pili (Uf. 21: 8).

5. *Waovu wataangamizwa.* Waovu wote wataangamizwa (Zab. 145: 20), Mapepo yalipata kuuliza, je umekuja kutuangamiza? (Mk. 1: 24). Tena waovu wataadhibiwa kwa maangamizi ya milele (2Thes. 1: 9). Hata Ibilisi naye ataharibiwa (Ebr. 2: 14)

Maelezo ya waandishi waliovuviwa kwingine walitumia misemo mikali. Kwamba siyo tu waovu watachomwa, (Uf. 19: 20, 21) bali pia watateketezwa (2Pet. 3:10). Siyo tu wataangamizwa (Mt. 21: 41, Mk. 1:24) bali pia wataangamizwa na kutengwa (Mdo. 3:
23), Siyo tu watatoweshwa (Zab. 104: 35 Zab. 37: 20), bali pia watatoweshwa kwa utisho (Zab. 73: 19). Hivyo ndivyo Biblia isemavyo juu ya adhabu ya waovu.

Vielelezo hufafanua mwisho wa Waovu

Lugha inayoelezea hatma ya waovu iko wazi. Waovu wanafananishwa na vinavyowaka yaani makapi (Zab. 1: 4) mabua (Isa. 40:24) na makapi yatakayoteketezwa (Mal. 4: 1)

Kama ilivyoangamizwa Sodoma na Gomora ndivyo itakavyokuwa kwa waovu. Miji ilipinduliwa (Kumb. 29: 23, Isa. 13: 19). Na kwamba iliangamizwa (Mw. 19: 29). Maangamizi yalikuwa makamilifu kwa kuwa tunasoma waliangamia wote (Luk. 17: 29)

Maangamizi ya Sodoma hayakuwa ya muda mrefu kwa kuwa Biblia inasema yalikuwa kama ya dakika moja (Maombolezo 4: 6). Zaidi, yaliangamizwa yakabaki majivu (2Pet. 2:6). Yuda, anasema adhabu ilikuwa ya moto wa milele (Yuda 7). Hii haiwezi kumaanisha moto ambao unaowaka milele bila kwisha, kwa kuwa ile miji haiendelei kuwaka moto leo. Hivyo, moto unaosemwa hapa ni wa milele kwa matokeo yake; yaani matokeo ya maangamizi yalikuwa ya kudumu.

Je, 'daima' au 'milele' yaweza kumaanisha isiyo ya kudumu?

Matumizi ya neno daima au milele laweza kuwa na kikomo. Tutazame mafungu machache: -

Pasaka ilipaswa kuadhimishwa milele (Kut. 12: 17). Mtumwa aliyekubali alipaswa kumtumikia bwana wake milele (Kut. 21: 6), Mtoto Samweli alipaswa kuhudumu hekaluni milele (1Sam.1: 22), Yona alikaa kwenye tumbo la samaki milele (Yon. 2:6) na ukoma ulipaswa kutomwacha Gehazi na uzao wake milele (2 Waf. 5:27). Filemoni naye katika agano jipya aliombwa kukaa na Onesmo milele. (Filem. 15). Kwa hiyo ukombozi wa milele (Ebr. 9:12) na hukumu ya milele (Ebr. 6:2) ni maelezo yanayoelezea ukamilifu wa ukombozi na ukamilifu wa hukumu katika matokeo; siyo katika mchakato. (Angalia pia Uf. 19: 3, Uf. 20:10, Uf. 14: 11 Zab. 92: 7). Misemo hii mikali yaweza tu kueleweka kwa mtazamo wa Isaya 34: 8 – 10) "Maana ni siku ya kisasi cha Bwana, mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni. 9 Na vijito vyake vitageuzwa kuwa lami, na mavumbi yake yatageuzwa kuwa kiberiti, na ardhi yake itakuwa lami iwakayo. 10 Haitazimwa mchana wala usiku, moshi wake utapaa milele; tangu kizazi hata kizazi itakuwa ukiwa; hapana mtu atakayepita kati yake milele na milele"

Sababu za kukataa mateso ya milele

1. Kwa sababu uzima wa milele ni karama kutoka kwa Mungu (Rum. 6: 23). Waovu hawataona uzima (Yoh. 3: 36). Hakuna muuaji aliye na uzima wa milele (1Yoh. 3: 15).
2. Kwa sababu mateso ya milele yatadumisha matokeo ya dhambi, vilio, machozi na masikitiko ambavyo ni kinyume na Uf. 21: 4 inayosema havitakuwako.
3. Kwa sababu kuwa na kisehemu chenye watu wanaoteseka milele kutatia doa kwenye ulimwengu wa Mungu na itaonekana Mungu hawezi kuondosha doa hilo.
4. Kwa sababu mawazo ya watakatifu yataondoshwa kwenye tabia ya Mungu ya upendo na badala yake yataelekezwa kwenye ghadhabu ya Mungu isiyoweza kutulizwa.
5. Kwa sababu Maandiko Matakatifu hufundisha kwamba kazi ya kafara ya Kristo ni kufutilia mbali dhambi (Ebr. 9: 26) kwanza katika wanadamu na baadaye katika ulimwengu. Ukamilifu wa kile ambacho kafara ya Yesu imefanya kitaonekana siyo tu kwa wanadamu waliokombolewa, bali pia katika ulimwengu ulioumbwa upya (Ef. 1: 14)